RIPOTI MAALUM

## *KINYESI CHA KUKU

# Lulu mpya katika ufugaji wa samaki na kilimo cha mboga

Na Sanula Athanas

## ■Mnufaika: Nina gari na nyumba za kisasa kwa wake zangu wote...

UNAPOKANYAGA Mtaa wa Kiebikiri ulioko Kata ya Turwa wilayani Tarime mkoani Mara, katika orodha ya wajasiriamali wake, hakosekani Christopher Mwita mwenye umri wa miaka 48.

Mahali hapo ni umbali wa Km 4.3 kusini mashariki mwa Mji wa Tarime na safari yake kutoka mjini ni mwelekeo wa kufuata barabara ya lami ya Nyamwaga, kisha unachepuka kushoto ukipita kwenye barabara ya vumbi umbali wa mita 400 kulifikia shamba lake kutoka Shule ya Sekondari Mwera Vision inapoanzia barabara hiyo ya vumbi.

Kwa mbali anaonekana Mwita akiwa katika harakati za kuhudumia mifugo yake kwenye eneo ambalo maji yake ni ya chemchemi.

Uso wake umejawa tabasamu lenye mzizi wa mafanikio aliyoanza kuyashuhudia miaka 14 iliyopita katika shughuli zake za ufugaji mseto unaojumuisha kuku, samaki na bustani ya migomba na mboga (mchicha, sukumawiki, chinese na kunde).

Kinachoshuhudiwa katika mradi wake huo ni ujasiriamali usiozoeleka kwa wengi, kuku, samaki na bustani vinaendeshwa kwa wakati mmoja, eneo moja, vinategemeana na kila kimoja kikiwa na mazao maradufu ya kawaida.

Leo hii maisha ya Mwita, ambaye awali alikuwa akiendesha uzalishaji wa bidhaa hizo kienyeji, baadaye akapata darasa na kuthubutu kujitosa kwenye teknolojia hiyo mpya, yamekuwa yenye kicheko cha kudumu.



Mjasiriamali Christopher Mwita (kulia) akiwa kazini na vijana wake.

Uzalishaji wa samaki na kuku sasa umemwongezea theluthi mbili ya ilivyokuwa awali. Jicho zaidi likizama kwenye uchumi huo penye ubia wa samaki na bustani, penyewe pametikisa zaidi pakiwa na ongezeko linalokita asilimia 300.

Maisha yake kwa ujumla si haba. Pato lake kwa mwaka lina wastani wa mara mbili ya alivyokuwa zamani, huku akijidai kwa miliki ya nyumba mbili mpya, kila mama mtoto na yake, mwenyewe akizunguka hapa na pale akiwa ameshikilia usukani na kupiga honi mitaani, jambo ambalo awali lilikuwa tamthilia isiyo na ushuhuda halisi kwake.

### YAMEWEZEKANAJE HAYO?

Mjasiriamali Mwita anasimulia kwamba ni matokeo ya kile alichokianza mwaka 2004, lakini sura kubwa ya mafanikio ilijitokeza mwaka 2007 baada ya kupata darasa lililojitosheleza na kuibua majibu chanya yaliyoangukia hata kubadili haiba ya maisha yake ya kawaida.

Hiyo ilianza pale Mwita alipokuwa mnufaika wa mafunzo maalum ya ubunifu kutoka Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI), hata yakamwezesha kupanua ufugaji wake kwa haraka pale mwaka 2004 yalipomwondoa kutoka kwenye ufugaji wa kienyeji, akiwa na bwawa la samaki lenye ukubwa wa mita za mraba 30 (mita tano kwa sita) na ndani ya mwaka mmoja akapanua kufikia mita za mraba 120 (mita 10 kwa 12), ambazo ni mara nne ya awali.

Mwita mwenye wake wawili na watoto sita (watatu wa kike), anasema alizidi kusonga mbele, akiainisha kutoka mwaka 2005 alipojitanua zaidi hadi kufikia bwawa lenye ukubwa wa mita za mraba 380 (mita 19 kwa 20). Hatua hiyo ya upanuzi wa mradi wa mabwawa, aliifanya kwa mtindo tofauti kidogo wa kuongeza mabwawa mengine mawili mapya, kila moja likiwa ni kubwa zaidi kuliko ya awali.

Anafafanua hali ya mabwawa hayo kwamba moja lina ukubwa wa mita za mraba 400 (mita 20 kwa 20) na lingine lenye ukubwa wa mita za mraba 450 (mira 15 kwa 30), ambayo kwa ujumla wake yameunda tafsiri mpya ya mafanikio yake kwenye ujasiriamali huo, yakiwa na muundo na mfumo wa uzalishaji mpya.

### UNAVYOENDESHWA

Kuhusu namna ya uzalishaji anaouendesha, Mwita anasema: "Kinachofanyika hapa unakuwa na bwawa la samaki, juu yake unajenga banda la kuku na pembeni ya bwawa unakuwa na bustani. Kinyesi cha kuku kikidondoka kwenye maji, kinakuwa chakula adhimu kwa ajili ya ukuaji wa samaki. Maji nayo yanapata rutuba inayomwagiliwa kwenye bustani.

"Muhimu hapo, hakikisha banda lako la kuku halisogei sana kwenye maji, walau mita moja na nusu au mbili kutoka kwenye maji maana usiku kunakuwa na baridi sana kwenye bwawa. Kuku wakipigwa na baridi kali, wanakonda. Wakikumbwa na hali hiyo, hutapata mayai. Pia ni muhimu kuweka uzio kuzungushia bwawa kwa ajili ya usalama wa samaki na kuku.

"Wakati ninaanza ufugaji mseto mwaka 2004, baadhi ya majirani waliniona kama nimepatwa na kichaa, lakini baada ya mafanikio wamekuwa miongoni mwa watu wengi wanaofika hapa kuja kujifunza na hata kununua kuku, samaki, mboga na ndizi.

"Nimekuwa nikipata wageni wanaokuja kujifunza kutoka mikoa ya Tabora, Arusha, Shinyanga, Dar es Salaam, Pwani, Mbeya na hata wanaotoka Uganda, na nimeitwa maeneo mengi kwenda kutoa elimu hii.

"Kwa kifupi, huu ni ufugaji wa gharama nafuu sana. Ninalisha kuku, kuku wanalisha samaki! Maji haya yenye rutuba yanatumika kumwagilia bustani, mazao ya bustani nayo yanakuwa chakula kwa hao wawili (kuku na samaki) na vyote hivyo unaweza kuvuna na kuuza. Shughuli inajiendesha yenyewe bila ya gharama kubwa.


"Wateja wangu ni wa hapa hapa Tarime, huwa ninauza bidhaa hapa hapa shambani kwangu. Wanunuzi wa jumla wa samaki na kuku huwa wanakuja ninawauzia, wao wanakwenda kuuza huko wanakojua."

Ndani ya falsafa ya kila mafanikio kuna magumu yake, hilo pia linajitokeza kwenye uzalishaji huo ambao Mwita anautolea ufafanuzi:

"Kikwazo katika mradi huu kwa sasa ni kwenye upatikanaji wa mbegu. Vifaranga vya samaki vinapatikana Arusha, Kenya na Uganda. Pia kunapokuwa na ukame, wale 'ndege mwarabu' wanakuja kwa ajili ya kusaka chakula, wanatua kwenye bwawa na kuchukua samaki.

"Kunapokuwapo kenge pia ni tatizo. Kuna shida ya vyura na nyoka, kunapokuwa na vyura ndani

INAENDELEA UK 5



Bustani ya mjasiriamali huyo inayotumia maji ya ufugaji mseto.



Mwonekano wa mradi wa ufugaji mseto unaofanywa na mjasiriamali huyo mjini Tarime. PICHA ZOTE: SANULA ATHANAS